TANGAZO LA SERIKALI NA. 689 la tarehe 15/9/2023

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)

SURA YA 288

# SHERIA NDOGO

*(Imetungwa chini ya Kifungu cha 89)*

MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA (AFYA NA USAFI WA MAZINGIRA) YA HALMASHAURI YA MJI WA BUNDA YA MWAKA 2023

Jina

TS Na.375
27/5/2022

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Marekebisho ya Sheria Ndogo ya (Afya na Usafi wa Mazingira) ya Halmashauri ya Mji wa Bunda ya Mwaka 2023, na itasomwa kwa pamoja na Sheria Ndogo ya (Afya na Usafi wa Mazingira) ya Halmashauri ya Mji wa Bunda ya Mwaka 2022 ambayo hapa imerejewa kama "Sheria Ndogo Kuu".

Marekebisho Kifungu cha 15

2. Marekebisho yamefanyika katika Kifungu cha 15 cha Sheria Ndogo Kuu kwa kukifuta na kuandika upya ili kisomeke kama ifuatavyo:
   "itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayeendesha biashara ya vyakula vya kupikwa au kukaangwa kuhakikisha kwamba vyakula hivyo vinahifadhiwa kwenye sanduku safi lililowekwa kioo kuzuia nzi au vumbi au wadudu waletao madhara kwa afya ya binadamu ".

Marekebisho ya Jedwali la Kwanza

3. Marekebisho yamefanyika katika Jedwali la Kwanza kwa kufuta rejea ya Kifungu cha "25" na badala yake kuweka rejea ya Kifungu cha "26".

Marekebisho ya Jedwali la Pili

4. Marekebisho yamefanyika katika Jedwali la Pili kwa kufuta rejea ya Kifungu cha "31(1)" na badala yake kuweka rejea ya Kifungu cha

"32(1)".

Marekebisho ya Jedwali la Tatu

5. Marekebisho yamefanyika katika Jedwali la Tatu kwa kufuta rejea ya Kifungu cha "45" na badala yake kuweka rejea ya Kifungu cha "46".

Marekebisho ya Jedwali la Nne

6. Marekebisho yamefanyika katika Jedwali la Nne kwa kufuta rejea ya Kifungu cha "47(1)" na badala yake kuweka rejea ya Kifungu cha "48(1)".

Marekebisho ya Jedwali la Tano

7. Marekebisho yamefanyika katika Jedwali la Tano kwa kufuta rejea ya Kifungu cha "52" na badala yake kuweka rejea ya Kifungu cha "53".

Dodoma,
Agosti, 2023

ANGELLAH JASMINE KAIRUKI (MB)
*Waziri wa Nchi - Ofisi ya Rais*
*(Tawala za Mikoa Na Serikali za Mitaa)*